



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**



**TANGAZO LA KOZI MAALUM YA MAOPARETA WA MITAMBO YA KAZI ZA UJENZI
(GRADER OPERATOR' COURSE)**

1. Utangulizi

Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi “Institute of Construction Technology” (ICoT) ni Taasisi iliyo chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi yenye makao makuu katika Mkoa wa Morogoro kilipokuwa Chuo cha Ujenzi. Taasisi inawatangazia wananchi wote kuwa inatarajia kuendesha kozi maalum ya Maopareta wa Mitambo “Grader Operators’ Course” ya Kazi za Ujenzi na Matengenezo ya Barabara kama ifuatavyo: -

	Jina la kozi	Muda wa Mafunzo	Mafunzo yatafanyika
1	Kozi Maalum ya Maopareta wa Greda (Motor Grader Operators’ Course).	Wiki Kumi (10) 28/11/2022 – 03/02/2023	Mkoani Morogoro (ICoT – Morogoro)

2. Masomo Yatakayofundishwa

Washiriki watajifunza moduli mbali mbali zinazohusu uendeshaji na utunzaji wa mitambo kama ifuatavyo: -

- i. Kudumisha na kuweka usalama wa Mitambo na mahali pa kazi;
- ii. Uendeshaji na Utumiaji wa Greda katika kazi za Ujenzi na Matengenezo ya Barabara;
- iii. Kufanya Ukaguzi na Matengenezo ya awali ya Mitambo; na
- iv. Kuweka kumbukumbu za Utunzaji wa Mitambo.

3. Njia za Ufundishaji

Mafunzo yatafanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza itakuwa ni mafunzo ya nadharia (Darasani) kwa muda wa wiki tatu (3) na awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo (‘Site’) kwa muda wa wiki saba (7).

4. Lugha ya Mafunzo

Lugha itakayo tumika katika kozi maalumu ya Maopareta wa Greda (Motor Grader Operators’ Course) itakuwa ni ya mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

5. Malengo ya Kozi

Kozi hii inalenga kumpatia mshiriki uwezo na ujuzi wa kutumia Greda (Motor Grader) katika kufanya kazi za Ujenzi na matenegenzo ya Barabara na mwisho wa kozi tunatarajia Mshiriki atakuwa na uwezo wa: -

- i. Kutumia Greda (Motor Grader) katika kufanya kazi ya ujenzi na matengenezo ya barabara;
- ii. Kuhakiki usalama mahala pa kazi na utunzaji wa mtambo (Greda);
- iii. Kufanya matengenezo ya awali pindi inapotokea hitilafu na kutunza kumbukumbu za mtambo - Greda.

6. Sifa za Muombaji

Muombaji anatakiwa kuwa na cheti cha kidato cha nne (Form IV) pamoja na leseni ya udereva.

7. Gharama za Mafunzo

Gharama za kushiriki mafunzo ni shilingi za Tanzania Milioni Moja (1,000,000) tu ambazo zitagharamia ada ya ushiriki, Vitini pamoja na vifaa vya mafunzo, chai ya asubuhi na chakula cha mchana. Mshiriki atajitegemea huduma nyingine zote muhimu ili kuweza kushiriki mafunzo kikamilifu.

8. Namna ya Kutuma Maombi

Kwa Tangazo hili, Wale wote wenye sifa zilizoanishwa hapo juu na watakao hitaji kupata mafunzo haya watume maombi yao katika Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi ICoT Makao Makuu – Morogoro au Tawi la Mbeya (ICoT – Mbeya) kwa kutumia anuani ya Posta, barua pepe, au kwa kupiga simu kwa namba zilizotolewa hapa chini. Malipo ya Ada yalipwe kabla ya wiki mbili ya kuanza kozi kwa kutumia 'control number' itakayotolewa kwa mshiriki yeyote atakayehitaji kupata mafunzo.

WASILIANA NASI **MKUU WA TAASISI**

Institute of Construction Technology
ICoT,
S.L.P 1957,
MBEYA.

Simu : 025 295 7484/5
: 0764775354/0769317404
Nukushi : 025 295 7486
Barua pepe : attimbeva@mow.go.tz,
attimbevafrica@gmail.com

Institute of Construction Technology
ICoT,
S.L.P 963,
MOROGORO.

Simu : 023- 2935229/023- 2935226
: 0787059555 /0786384062/0629782068
Nukushi : 023-2935227
Barua pepe : mwti@morogoro.net